



TANGAZO KWA UMMA

**MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAREKEBISHO YA BEI ZA
HUDUMA ZA UMEME ZINAZOTOLEWA NA MWENGA POWER
SERVICE LIMITED KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021/22-2023/24**

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-E-21-001

Mnano Machi 2021, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilipokea maombi kutoka Mwenga Power Service Limited (MPL) juu ya marekebisho ya huduma zake kwa kipindi cha mwaka 2021/22 -2023/24. Bei zinazopendekezwa na ada mpya ya maunganisho ni kama inavyoonyesha kwenye jedwali 1 na 2 hapo chini.

Jedwali 1: Bei za Umeme za Sasa na Zilizopendekezwa (Shilingi/Uniti)

Makundi ya Wateja	Kipengele	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa		
		2020/21	2021/22	2022/23	2023/24
D1	Malipo ya Nishati (0- 50 Uniti/mwezi)	60	100	100	100
	Malipo ya Nishati (Zaidi ya 50 uniti/mwezi)	273	350	350	350
T1	Malipo ya Nishati	234.04	292	292	292

Jedwali 2: Ada ya Maombi ya Sasa na Zinayopendekezwa ya Huduma za Njia za Huduma

Kipengele	Bei za Sasa (TZS)	Bei Zinazopendekezwa (TZS)
Ada ya Maombi	5,000	0
Maombi yote Mapya		
Gharama Mpya ya Laini za Huduma		
(A) Gharama Zaidi Laini za huduma-Awamu moja (mita 30)		
D1 na Mita ya M-LUKU	150,000	150,000

Kipengele	Bei za Sasa (TZS)	Bei Zinazopendekezwa (TZS)
T1 na Mita ya M-LUKU	150,000	25,000
(B) Gharama Zaidi Laini za Huduma – Awamu tatu (mita 30)	380,000	150,000
T1 na Mita ya LUKU (16 mm ² cable)		
(C) Awamu moja mita 70	850,000	850,000
Urefu njia moja mita 70 pamoja na nguzo 1 (LUKU)		
(D) Awamu tatu mita 70	1,300,000	1,300,000
Urefu njia tatu mita 70 pamoja na nguzo 1 (LUKU)		

Angalizo: Tozo hizi hazijajumuisha kodi yoyote

Kulingana na MPL, sababu ya msingi ya kuomba mapitio ya bei za huduma za umeme ni kutokana na bei za sasa za MPL zililinganishwa na bei za TANESCO za mwaka 2012 kwa kuwa wakati huo MPL hakuwa na taarifa za utendaji na hivyo hazikuzingatia gharama. MPL imeeleza kuwa bei zitakazoidhinishwa zitadhihirisha kuwa sekta binafsi, inayodhibitiwa na yenye mtandao uliunganisha wateja wa vijijini kwenye gridi inaweza kuwa endelevu kiuchumi na wakati huohuo ikiendelea kuongeza wateja wapya na kiwango cha matumizi ya umeme kwa kila mteja.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 19 (2) (b) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, kutakuwa na mkutano Jumatatu, tarehe **14 Juni 2021 katika Ukumbi wa Ofisi ya Kijiji cha Igoda Mufindi kuanzia saa 4:00 asubuhi**. Lengo kuu la mkutano huo ni kukusanya maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), Baraza la Ushauri la Watumiaji (CCC), wateja na umma kwa jumla juu ya uhalisia wa maombi ya mabadiliko ya bei zinazopendekezwa.

Wale wote ambao wanataka kuwasilisha maoni ya maandishi kuhusu bei zilizopendekezwa wanaalikwa kufanya hivyo kwa kuandika kwa Mkurugenzi Mkuu kwa kutumia anwani hapo juu wakati wowote ifikapo tarehe **15 Juni 2021. Maelezo zaidi juu ya mapendekezo ya bei zilizowasilishwa na MPL yanaweza kupatikana kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Ofisi Kuu, Nyumba ya EWURA, Plot No 3, Block AD, Medeli West. SLP 2857, Dodoma.**

**Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)**



**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
3 Juni 2021**